



Afrika

Kutumia dawa za kulevya ni shuari! Hauwezi kupata Ukimwi ukitumia dawa za kulevya.

Laa! Dawa za kulevya zamfanya mtu kuchukuwa uamuzi mbaya. Zaweza kukufanya ukachukua hatuwa mbaya kama kufanya mapenzi bila kinga au kushiriki kwa utumiaji wa sindano.

Kufanya mapenzi na watu wengi au msichana bikira huponya ukimwi na magonjwa mengine ya zinaa.

Laa! Kufanya mapenzi ovyo ovyo ama na msichana bikira kwaweza kuwaambukiza wote. Ukiendelea kufanya mapenzi ilhali una ukimwi au magonjwa ya zinaa, tumia kinga. Utumiaji wa dawa za kulevya ukiwa umeambukizwa, waweza kusambaza ukimwi na magonjwa mengine ya zinaa kwa ajili ya uamuzi mbaya kwa mfano kufanya mapenzi bila kinga au kwa utumiaji wa sindano zilizotumiwa na wengine.

Ukimwi ni ugonjwa wa shoga pekee yao.

Laa! Ukimwi haubagui kati ya watu. Huku Afrika kwa mfano, ukimwi huambukizwa kutoka kwa mwanaume hadi kwa mwanamke au kutoka kwa mwanamke hadi kwa mwanamume wanapofanya mapenzi.

Kuna dawa ya kuponya ukimwi.

Laa! Hakuna dawa ya kuponyesha ukimwi. Kwenye sehemu zingine za dunia, dawa za kuwasaidia walioambukizwa kuendelea kuishi maisha sahihi zapatikana, lakini ni ghali na zahitaji kutumiwa bila kukoma. Utumiaji wa kinga au kutotumia dawa za kulevya ndio namna za kujikinga kutokana na ukimwi.

Ninaweza kuambukizwa ukimwi kwa kuketi karibu na mtu aliyeambukizwa ukimwi.

Laa! Huwezi kuambukizwa ukimwi kwa kuketi karibu na mtu aliyeambukizwa. Huwezi pia kuambukizwa kwa kutumia vyombo vya chakula, kutumia choo au kwa kumguza mtu aliyeambukizwa. Ukimwi unasambazwa kwa njia zifuatazo:

1. Kwa njia ya utumiaji wa sindano au kupewa damu.
2. Ukifanya mapenzi na mtu aliyeambukizwa bila kinga.
3. Kutoka kwa mama mja mzito aliyeambukizwa hadi kwa mtoto wake, kabla ya kuzaliwa, anapozaliwa au anaponyonya.

Ni vigumu sana kuambukizwa virusi vya ukimwi na wanawake wanene, wanawake walioolewa au wanafunzi wa kike.

Laa! Mtu yeyote aweza kuambukizwa na ukimwi bila kubagua baina ya unene, kama umeowa au kuolewa, miaka, dini, rangi au urathi. Umjuwe mwenzako mbele ya kufanya mapenzi. Jihifadhi dhidi ya ukimwi kwa kutumia kinga unapo fanya mapenzi, usitumie sindano ila ikiwa mpya na usichukuwe uamuzi mbaya ukiwa umetumia dawa za kulevya.

Wacheni mila potofu